



KUTANA NA PAWARISA

Kumfuata Yesu huko **Thailand**

Jinsi Pawarisa Anavyomfuata Yesu

Pawarisa anamwalika binamu yake aende kanisani pamoja naye. Binamu anapokuja, Pawarisa anamsaidia ahisi kukaribishwa. Anamsaidia akutane na watoto wengine katika Msingi na kupata marafiki.

Nyumbani, Pawarisa anasaidia kwa kusafisha chombo cha chakula na viatu vyake. "Ninaburudika wakati ninaposaidia," Pawarisa anasema. Anaishi na shangazi na bibi yake na anapenda kuwasaidia. Pia hukunja blanketi lake kila asubuhi.

Mama yake Pawarisa amefariki karibuni. Wakati Pawarisa anapomkumbuka mama yake, shangazi yake humsaidia asali kwa Baba wa Mbinguni. Anahisi kupendwa baada ya kusali. "Ninaposali, ninahisi kama vile Yesu yupo nami," anasema. ●



Pawarisa akiwa na bibi na shangazi yake.

Wewe Pia Unaweza Kumfuata Yesu!

Ni kipi umefanya ili kumfuata Yesu? Andika na utueleze! Nenda kwenye jalada la nyuma ili kuona jinsi ya kufanya hilo.



สวัสดี!



Kuhusu Pawarisa

UMRI MIAKA: 7

ANATOKEA: Nonthaburi, Thailand

LUGHA: Kithai

LENGO: Kuwa mbunifu wa ndani na kupamba vyumba katika nyumba na majengo.

MAMBO YA KUPITISHA MUDA: Dansi, kuendesha baiskeli, kujifunza kinanda, kuogelea, kusoma na taekwondo

FAMILIA: Pawarisa, shangazi na bibi

Mambo Ayapendayo Pawarisa

HADITHI ZA YESU: Wakati alipobatizwa (ona Mathayo 3:13-17)

MAPUMZI AU UTAMADUNI WA FAMILIA: Kristmasi na safari za familia

TUNDA NA MBOGA: zabibu za kijani na matango

RANGI: Zambarau

WIMBO WA MSINGI: "I Love to See the Temple" (Kitabu cha Nyimbo za Watoto, 95)